ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001: 2015 Certified

HALIUZWI

Newsletter

SEPTEMBA 2019

ISSN 1821 - 7273 TOLEO NA. 25

EWURA yanyakua mshindi bora wa pili 88 Simiyu

Kauli Mbiu: *"Udhibiti wa Haki kwa Matokeo CHANYA - IMPACT"*

BODI YA WAHARIRI

MWENYEKITI
Bw. Nzinyangwa Mchany

MHARIRI
Bw. Titus Kaguo

MHARIRI MSAIDIZI
Bw. Wilfred Mwakalosi

WAANDISHI
Bi. Asiatu Msuya
Bi. Tobietha Makafu

MAKAO MAKUU YA EWURA
Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF,
Barabara ya Makole,
S.L.P. 2857,
Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002-3,
Nukushi: +255 26 2329005,
Barua pepe: info@ewura.go.tz

www.ewura.go.tz

YALIYOMO

Kutoka kwa Mhariri 3

EWURA yanyakua mshindi bora wa pili 88 Simiyu 4

10 mbaroni kwa tuhuma za uuzaji holelala wa mafuta 5

Ewura yajibu hoja za watumiaji 600 maonesho ya Sabasaba 6

EWURA yaondosha biashara haramu ya LPG mtaa maarufu wa Dar 7

Mafanikio zaidi udhibiti sekta ya umeme kwa zaidi ya 600 kupewa leseni 8

Watanzania wengi zaidi wafaidika na Gesi ya Kupikia majumbani 9

Leseni za ufungaji umeme zaboreshwa zaidi 10

PICHA YA MBELE:
EWURA yanyakua mshindi bora wa pili kwenye Maonesho ya 88 Simiyu.

Kutoka kwa Mhariri

Titus Kaguo

Wapenzi Wasomaji Wetu!

Kwa niaba ya Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na kwa unyenyekevu, ninawakaribisha wote katika Jarida la EWURA, Toleo 25 katika mfululizo wa machapisho ya Majarida ya Mamlaka.

Jarida hili linakuja wakati EWURA ikiwa inafanya kazi kutoka Dodoma na ikiwa imetengemaa baada ya kuhamia kutoka Dar es Salaam April 9, 2018

Tangu tuhamie Dodoma na tofauti na matarajio yetu, EWURA imetekeleza majukumu yake ya kiudhibiti kwa mafanikio kama ilivyokuwa ikifanya wakati Makao Makuu yalipokuwa Dar es Salaam ambako ndiko kwenye watoa huduma wengi.

Sasa kibinafsi na kwa heshima nawakaribisha kusoma taarifa za kuvutia zilizotokana na shughuli zetu zilizotekelezwa na EWURA katika kipindi cha mwezi Julai na Septemba 2019.

EWURA inadhibiti kiufundi na kibiashara sekta ndogo tatu za Nishati ambazo ni Petroli; Umeme na Gesi Asilia na Sekta moja ya Maji; Maji na Usafi wa Mazingira.

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2019, EWURA ilifanya shughuli mbalimbali za kiudhibiti ambazo baadhi yake, zimechapishwa katika toleo hili, ambalo linachapishwa katika kutekeleza matakwa ya Sheria ya EWURA Sura na 414 ya Sheria za Tanzania, kipengele cha 6(e)

Kipengele cha 6(e) cha Sheria ya EWURA, kinasema kwamba ni wajibu wa Mamlaka kuhakikisha inaboresha ustawi wa jamii ya Watanzania kwa kuimarisha elimu kwa umma, ufahamu na uelewa wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa pamoja na; haki na wajibu wa walaji na watoa huduma wa sekta zinazodhibitiwa; Njia za kutatua migogoro na kusikiliza malalamiko, kazi na shughuli za mamlaka kwa ujumla.

Toleo hili linakuletea baadhi tu ya habari mbalimbali zilizotokana na utendaji wa shughuli za kiudhibiti kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2019 ambapo kutoka na muda na nafasi ya Jarida, Mamlaka imeshindwa kukuletea taarifa zote kwenu. Furahia usomaji wa Jarida letu na karibuni sana!

EWURA yanyakua mshindi bora wa pili 88 Simiyu

Na Tobietha Makafu

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati Maji (EWURA), imepata tuzo ya ushindi wa pili katika maonesho ya kitaifa ya wakulima, maarufu kama Nane Nane katika kundi lililoshindanisha taasisi za udhibiti, katika maonesho yaliyofanyika kitaifa viwanja vya Nyakabindi, Bariadi, mkoani Simiyu.

Tuzo hiyo iliyotolewa na Waziri Mkuu, Mh. Kassim Majaliwa katika kilele cha Nane Nane, Agosti 8 mwaka huu, ni matokeo ya huduma nzuri na elimu bora, juu ya udhibiti wa huduma za nishati na maji. Tuzo hiyo ilipokelewa na Meneja wa Kanda ya Ziwa, Bw. George Mhina.

Akizungumzia ushindi huo Bw. Mhina alisema: “EWURA imejikita kuhakikisha inatoa elimu kwa umma, ili watumiaji wa huduma za nishati na maji wapate kujua haki na wajibu wao katika matumizi ya huduma hizo.”

Bw. Mhina alisema tuzo hiyo ni kielelezo cha huduma bora ambayo EWURA inatoa katika maonesho, “hivyo tutajitahidi kuhakikisha huduma bora inaendelea kutolewa hata katika ofisi zetu za kanda na makao makuu na kuwaridhisha wateja wetu wote.”

Pamoja na kutoa elimu kwa umma, pia maonesho hayo yamekua ni sehemu ya kupokea maoni, malalamiko ya wateja na watoa huduma, maombi ya leseni za umeme kutoka kwa mafundi umeme na kutoa maelezo na ushauri kwa wawekezaji mbalimbali wa umeme na vituo vya mafuta.

Mbali na ushiriki wa EWURA Kanda ya Ziwa katika maonesho haya ya kitaifa, pia ofisi nyingine za kanda zilishiriki katika maeneo yao ambapo EWURA kanda ya kati ilishiriki maonesho hayo mkoani Dodoma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilishiriki mkoani Mbeya na Kanda ya Mashariki ilishiriki mkoani Morogoro.

10 mbaroni kwa tuhuma za uuzaji holela wa mafuta

Na Wilfred Mwakalosi

WATU 10 wamekamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na biashara holela ya mafuta ya dizeli na petroli katika Wilaya ya Bagamoyo, eneo la Msata mkoani Pwani, katika msako uliofanyika hivi karibuni.

Msako huo ulifanywa na timu ya maofisa kutoka Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na EWURA. Zaidi ya lita 110 za mafuta aina mbalimbali zilikamatwa, pamoja na vyombo vitupu vya kuhifadhia mafuta, mabomba yanayoaminika ni maalum kwa kunyonyea mafuta na risiti za TRA.

Timu hiyo ilifanikiwa kubaini wafanyabiashara saba waliokuwa na mafuta na watatu waliokutwa hawana mafuta lakini wakiwa na chupa zilizokuwa na dalili za kuhifadhi mafuta.

Katika operesheni hiyo timu ya maafisa hao ilipima dizeli na petroli katika vituo viwili vya mafuta vya TPDC COPEC Segera na ENGEN Segera na mafuta ya dizeli aliyokutwa nayo mmoja wa watuhumiwa.

Kwa kutumia mashine maalumu kung'amua vinasaba katika mafuta ili kubaini kama mafuta yanayouzwa kwenye soko la ndani yana vinasaba vilivyowekwa na EWURA, matokeo ya vipimo hivyo yalionesha kwamba vituo vya mafuta viwili vilivyoko eneo la Segera yana vinasaba kwa viwango sahihi.

Kwa mujibu wa Kanuni za Kuweka Mafuta Vinasaba na Udhibiti wa Ubora, GN Na. 210, mafuta yote ya petroli, dizeli na taa yanayotumika katika soko la ndani huwekewa vinasaba ili kudhibiti vitendo vya ukwepaji wa kodi, uchakachuaji na uingizaji wa mafuta kutoka nchi za jirani kwa magendo.

Mafuta ambayo hayawekewi vinasaba ni yale yanayokwenda nchi za jirani na mafuta kwa ajili ya matumizi ya miradi maalum iliyosamehewa kodi kama vile migodi, ujenzi wa reli, ujenzi wa barabara n.k.

Ili mafuta yanayotumika katika soko la ndani yatambulike kuwa yamekidhi viwango vilivyowekwa na EWURA, ni lazima yawe na kiwango cha vinasaba ambacho ni 3PPM±7%. Kinyume chake, mafuta hayo yatakuwa yamechakachuliwa au yatakuwa yamepatikana kwa njia ambazo si halali na hata kutokulipiwa kodi na hivyo kuikosesha serikali mapato.

EWURA yajibu hoja za watumiaji 600 maonesho ya Sabasaba

Na Tobietha Makafu

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imetoa elimu na kuwafikia watu zaidi ya 600 katika maonesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es salaam DITF maarufu Sabasaba, yaliyofanyika kuanzia 28 Juni hadi 13 Julai, mwaka 2019. Maonesho hayo yaliyofunguliwa na Makamu wa Rais Mh. Samia Suluhu, na yalifungwa tarehe 13 Julai 2019 na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mh. Balozi Seif Ali Idd.

Maonesho hayo ya Saba Saba yalikuwa ni wasaa mzuri kwa EWURA kujibu na kufafanua masuala mbalimbali yaliyowasilishwa na watumiaji wa huduma za nishati na maji waliotembelea maonesho hayo.

Akielezea juu ya sababu za kubadilika kwa bei za mafuta, Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano EWURA, Bw. Titus Kaguo, alisema mabadiliko hayo yanatokana na hali halisi ya kupanda na kushuka wa bei za mafuta katika soko la dunia, hivyo kusababisha kupanda na kushuka kwa bei za mafuta hapa nchini pia.

Kuhusu upatikanaji wa mafuta maeneo ya vijijini, hasa baada ya kuongezeka kwa usafiri wa pikipiki maarufu kama bodaboda, Bwana Kaguo alisema EWURA imeandaa kanuni mpya za kuanzisha vituo vya mafuta vinavyoweza kuhamishika, ambavyo vinaweza kubebwa na vyombo vidogo vya moto kama malori au matrekta madogo, piki piki za miguu mitatu kwa ajili ya kuuza bidhaa hizo vijijini. Akijibu swali juu ya uwekezaji katika uzalishaji usambazaji na uuzaji sekta ya umeme, Bw. Kaguo alisema, EWURA inatoa leseni kwa wazalishaji wakubwa wanaozalisha umeme kuanzia Megawati 10 na zaidi, na wazalishaji wadogo kuanzia Megawati10 kwenda chini, uzalishaji unaweza kua wa umeme wa jua, upepo, maji na nyinginezo. Kwasasa wazalishaji wadogo wameweza kuzalisha jumla ya Megawati 60. Kuhusu umeme majumbani, Bw. Kaguo alisema, EWURA inatoa leseni kwa wakandarasi wote wanaofanya shughuli za ufungaji wa umeme, majumbani, viwandani na sehemu nyingine na mpaka sasa zaidi ya leseni 2300 zimetolewa kwa madaraja mbalimbali, kulingana na elimu na wasifu wa mhusika.

“Leseni hizi zinatolewa ili kuepusha fundi asiye na sifa kutokufanya shughuli za ufungaji umeme. Adhabu zinatolewa kwa fundi yeyote anayefanya kazi za ufungaji wa umeme bila leseni,” alisema.

Katika sekta ya maji, wananchi wengi walilalamikia ankara za maji, wakisema kuwa ni kubwa zaidi ya matumizi yao. Bw. Kaguo alisisitiza kwa malalamiko kama hayo na mengine katika sekta ndogo za umeme na petroli, wayafikishe katika ofisi za EWURA za kanda jirani na mlalamikaji. EWURA ina ofisi Dodoma, Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam), Kanda ya Kaskazini (Arusha) na Kanda ya Nyanda za juu Kusini (Mbeya.)

“Kila muuzaji wa gesi ya kupikia majumbani (LPG) lazima awe na mzani kwa ajili ya kupima mtungi na lazima uzito wa gesi na mtungi uwe kama ulivyoandikwa katika mtungi, pia mtungi ni lazima uwe na lakiri,” alisema Bw. Kaguo alipokua akitoa maelezo ya jinsi ya kukabiliana na wizi unafanyika katika gesi za kupikia majumbani.

Mwisho Bw. Kaguo alisisitiza wananchi kusoma mkataba wa EWURA wa huduma kwa mteja ambao umeandikwa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza, ukielezea wajibu wa EWURA, mteja na mtoa huduma ili wapate haki zao kwa usahihi.

EWURA yaondosha biashara haramu ya LPG mtaa maarufu wa Dar

By Wilfred Mwakalosi

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeondosha biashara haramu ya gesi ya kupikia (LPG) iliyokuwa inafanywa kinyume cha sheria katika mtaa maarufu wa Dar es Salaam, Ilala.

Biashara hiyo ilikuwa inahatarisha masuala ya Afya, Usalama na Mazingira (HSE) na kwa hivyo ilikuwa ni hatari kubwa. Zaidi ya hatari, imebainika kwamba vitendo vilivyokuwa vinafanywa kwenye biashara hiyo vilikuwa vinakwenda kinyume na sera ya ushindani wa kibiashara.

Katika msako wa hivi karibuni, mfanyabiashara wa gesi ya kupikia jijini Dar e Salaam, ajulikanaye kama Mafia Gas Mart alikutwa akitumia makazi ya watu huko Kariakoo mtaa wa Mafia, Nyumba Namba 55, Wilaya ya Ilala, kama hifadhi ya mitungi ya gesi ya LPG na pia kujaza gesi kwenye mitungi mingine kinyume cha sheria.

Kwa mujibu wa kifungu cha 179 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni ya 35 (1) ya Kanuni za LPG na tangazo la serikali namba GN 420, eneo hilo haliruhusiwi kutumika kwa kuhifadhi gesi ya kupikia na ni kosa kufanya hivyo. Kwa upande mwingine, kwa mujibu wa Kanuni ya 42 (1) ya Kanuni za LPG na tangazo la serikali GN 420, kitendo cha kujaza mitungi ya LPG ni marufuku na ni kosa, isipokuwa tu kwa ruhusa ya Mamlaka.

Msemaji wa EWURA Bw. Titus Kaguo anasema vitendo kama vilivyokuwa vinavyofanywa na Mafia Gas Mart (kuhifadhi mitungi ya LPG katika makazi ya watu na kuijaza gesi ya LPG) kunasababisha hatari kubwa kwa afya ya binadamu, usalama na mazingira.

“Inapotokea ajali ya moto, nyumba za maeneo ya jirani zitakuwa kwenye hatari kubwa,” alisema, na kuongeza kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 57 (1) na 60(1) ya Kanuni za LPG na tangazo la serikali GN 420, kikosi kilichohusika na ukaguzi kilikamata mitungi hiyo ya biashara haramu na kuwakabidhi kampuni zenye miliki ya majina yaliyokuwa kwenye mitungi hiyo kwa kuhifadhi hadi hapo suala hilo litakapotatuliwa. Eneo la tukio lilikutwa na mitungi ya makampuni mbalimbali ya gesi ya kupikia 147, kati ya hiyo 134 ikiwa mitupu, wakati iliyobaki ikiwa imejaa gesi. Mafia Gas Mart ilikutwa na mitungi ya gesi ya LPG ya wauzaji wa jumla ambao haikuwa imeingia nao mkataba wowote, kinyume na Kanuni ya 38 (1) ya kanuni za LPG na Tangazo la serikali namba GN 420, na ni kosa linalostahili adhabu.

Mkurugenzi wa Petroli Bw. Gerald Maganga, amesema ukaguzi wa namna hiyo ni sehemu tu ya zoezi kubwa la ufuatiliaji kwa nchi nzima ili kuhakikisha kuwa wadau katika sekta hii ndogo wanafuata sheria, taratibu na kanuni zilizopo.

Ujazaji wa gesi ya LPG unaofanywa kinyume cha sheria ukiwa umezingirwa na makazi ya watu na biashara nyingine, ni hatari kubwa kwa Afya, Usalama na Mazingira.

Mafanikio zaidi udhibiti sekta ya umeme kwa zaidi ya 600 kupewa leseni

Na Tobietha Makafu

Zaidi ya mafundi umeme 600 wanaofanya kazi za ufungaji umeme kwenye majengo wamesajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, na kupewa leseni za kuifanya shughuli hizo kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kwa mujibu wa ripoti ya sekta ya umeme kwa mwaka 2017/2018 iliyotoka hivi karibuni.

Kwa mujibu wa sheria ya Umeme (2008), mtu yeyote anayefanya shughuli za ufungaji umeme katika ngazi yoyote, awe na leseni ya EWURA, ili kuhakikisha shughuli hizo zinafanywa na wataalamu wenye uwezo stahiki kwa usalama wa watu na mali zao.

Kati ya leseni hizo 600 zilizotolewa, leseni 12 ni za daraja A, 52 daraja B, 225 daraja C, 255 Daraja D na leseni 56 Daraja W.

Pamoja na leseni hizo, pia EWURA imetoa leseni nyingine saba za wazalishaji wa umeme wenye uwezo wa kuzalisha jumla ya Megawati 97.3 kwa makampuni ya Dangote Cement Limited, Shanta Mine, Kagera Sugar, Ludewa Capacity Building, Mkonge Energy Systems na Ninety Two Limited.

Ripoti hiyo pia inaainisha kuwa EWURA imesajili kampuni za wazalishaji wadogo wa umeme, ambapo kampuni 10 ni za kuzalisha umeme wa jua na moja umeme wa maji.

Kwa ujumla zina uwezo wa kuzalisha Kilowati 453.03 zenye uwezo wa kuhudumia zaidi ya wateja 887 katika maeneo ambayo hakuna umeme wa TANESCO.

Katika kipindi cha mwaka 2017/2018, EWURA ilipokea jumla ya malalamiko 134 kuhusu ankara za umeme, madai ya fidia juu ya majanga ya moto na migogoro ya kukatiwa huduma, ambapo malalamiko 65 yalitatuliwa na mengine 69 yapo katika hatua ya kutafutiwa suluhu.

Pamoja na hayo ripoti pia imeainisha maendeleo katika kufanikisha malengo ya Taifa kwa kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme kwa asilimia 7.13, kuongezeka kwa njia za usafirishaji wa umeme na kuongezeka kwa wateja wapya kwa wastani wa asilimia 18.

Mafanikio katika sekta hii ya umeme yanatokana na kuongezeka elimu kwa umma, iliyoongeza kiwango cha ufahamu juu ya sekta hii ya umeme kwa watoa huduma na wateja.

Watanzania wengi zaidi wafaidika na Gesi ya Kupikia majumbani

Na Tobietha Makafu

Matumizi ya gesi ya kupikia majumbani yameongezeka kwa asilimia 33, kwa mwaka 2018, ikilinganishwa na matumizi hayo kwa mwaka 2017. Kuongezeka huko kumetokana na juhudi za serikali kutoa elimu kwa umma juu ya faida za matumizi ya gesi hizo dhidi ya matumizi ya mkaa na mafuta ya taa.

Hayo yamebainishwa na Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Bwana Titus Kaguo, alipokua akiongea na mwandishi wa habari hizi ofisini kwake jijini Dodoma hivi karibuni.

Bwana Kaguo alisema ongezeko hilo limetokana na wananchi wengi kuelewa umuhimu na unafuu wa gesi ya kupikia ukilinganisha na nishati nyingine ili kuendana na sera ya taifa ya nishati (NEP) ya mwaka 2015 inayosisitiza matumizi ya nishati mbadala ili kuboresha maisha.

Uagizaji wa gesi hiyo umeongezeka hadi kufikia tani 142,940 mwaka 2018, ambapo ni ongezeko la asilimia 33 ikilinganishwa na tani 107, 263 zilizoingizwa nchini kwa mwaka 2017. Haya ni mabadiliommakubwa katika matumizi ya gesi, hasa ikizingatiwa kwamba mwaka 2010 matumizi yake yalikuwa tani 20,000 tu.

Aidha pamoja na ongezeko hilo la gesi ya kupikia, Kaguo alisema bado maeneo mengi ya vijijini nishati hiyo haipatikani au wasambazaji wake ni wachache, hivyo wananchi wa maeneo hayo wanaendelea na matumizi ya kuni, mkaa na mafuta ya taa.

Leseni za ufungaji umeme zaboreshwa zaidi

Na Asiatu Msuya

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) sasa imerekebisha Kanuni za Ufungaji Umeme ili kuratibu vizuri zaidi masuala ya leseni na shughuli za ufungaji umeme nchini.

Kanuni hizo zilizochapishwa mwezi Mei, 2019 katika Gazeti la Serikali Namba 382 zimeboresha zaidi madaraja ya leseni za shughuli za ufungaji umeme kuwa nane kutoka 11 ya awali, na zimepandisha viwango vya misongo kwa kila daraja.

Gharama za maombi ya leseni, kunakilisha na kuhuisha leseni, ada na faini kwa wote watakaondesha shughuli za ufungaji umeme bila kuwa na leseni ya EWURA pia zimeanishwa katika kanuni hizo mpya.

Kanuni zimetaja sifa na viwango vya elimu na kuanisha masuala muhimu ya kuzingatia kwa wote wanaojishughulisha na ufungaji umeme. Masuala hayo ni:-

✓ Hairuhusiwi kufanya shughuli za Ufungaji umeme bila leseni ya EWURA na yeyote atakayekiuka ataadhibiwa vikali.

✓ Maombi ya leseni yatafanyika kieletroniki kwa kutumia kiungaishi kinachopatikana **www.ewura.go.tz.**

✓ Madaraja ya leseni na misongo yake ni A (misongo yote); B (misongo hadi volti 33,000); C (misongo isiyozidi volti 400); D (misongo isiyozidi volti 220); W (kufanya kazi zote kwa usimamizi wa A, B, C na D); na S kwa kazi maalumu yaani S1 (misongo yote), S2 (misongo isiyozidi volti 33,000 na S3 (misongo isiyozidi volti 1000).

✓ Leseni zitatolewa kulingana na madaraja husika kwa kukidhi kiwango cha elimu, uzoefu na ngazi ya taaluma ya ufundi umeme.

✓ Uhakiki wa maombi ya leseni utafanywa na jopo mahsusi ili kujiridhisha endapo yanakidhi vigezo na uhalali wa maombi pamoja na kuishauri Bodi kutoa uamuzi.

✓ Leseni zitakazotolewa kwa mafundi umeme zitadumu kwa kipindi cha miaka mitatu, au itakavyoonekana inafaa.

✓ Mwaombaji wa leseni atalipia leseni yake baada ya kuidhinishwa na kuichukua ndani ya kipindi kisichozidi miezi mitatu.

✓ Malipo ya leseni kwa madaraja ni :- Daraja A na S1 Tsh. 150,000/; Daraja B na S2 Tsh. 120,000/ Daraja C na S3 Tsh.100,000/; Daraja D Tsh. 60,000/ na Daraja W Tsh. 40,000/.

✓ Mamlaka inaweza kukataa kutoa leseni endapo itajiridhisha kuwa mwombaji ametoa taarifa za uongo au mgongano wa maslahi na kuwepo ukiukwaji wa sheria.

Gharama za maombi ya leseni, kunakilisha na kuhuisha leseni, ada na faini kwa wote watakaondesha shughuli za ufungaji umeme bila kuwa na leseni ya EWURA pia zimeanishwa katika kanuni hizo mpya.